JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

Telegrams: “NATIONAL FIRE”
Telephone: +255-22-2113537
Telefax: 255-22-2184569
Email: *muheza.tanga@frf.go.tz*

MKUU WA ZIMAMOTO (W)
MUHEZA,
JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI,
4 BARABARA YA MUHEZA
MKUMBI,
S.L.P 70,

Kumb Na. AB4.97/470/VI/17 **04.05. 2026.**

MWENYEKITI,
KAMATI YA USALAMA (W),
S.L.P 70,
MUHEZA.

TAARIFA YA JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI KWA KAMATI YA USALAMA YA WILAYA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRIL - 2026.

UTANGULIZI.

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Muheza linatekeleza majukumu yake yote kwa
mujibu wa sheria Na. 14,2007 ikiwa ni pamoja na Kuzima Moto, Kufanya ukaguzi wa
kinga na tahadhari ya moto unaoendana na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali na kutoa
elimu ya usalama wa moto kwa Umma.

RASILIMALI WATU.

Kituo kina jumla ya watumishi wanne (04), ambao ni Afisa (2) na NCOs (2).
Walioko kazini 03.

HALI YA MATUKIO

Kwa kipindi tajwa hapo juu kuliripotiwa taarifa ya tukio moja la moto wa Nyumba ya Makazi
(i)Moto wa Nyumba ya Makazi

Tukio la moto wa Nyumba ya Makazi lililotokea siku ya Jumanne ya tarehe 02.03.2026 Majira ya saa Sita mchana maeneo ya Kijiji cha Mkanyageni Kata ya Ngomeni Tarafa ya Ngomeni Wilaya ya Muheza inayomilikiwa na ndugu Salome Henry Ngunyali mwenye simu namba 0620388430,Kazi – Mwalimu,Kabila - Mbena,Dini – Mkristo,Umri -39 yenye ukubwa wa vyumba vitatu na sebule iliyokuwa ikiishi watu wanne Mume ,Mke ,Mtoto na Shemeji mtu ,hakuna madhara kwa Binadamu,Hasara ni kuungua kwa nyumba nzima na baadhi ya samani za ndani,Chanzo cha Moto huo ni hitilafu ya Umeme iliyoanzia kwenye Makutano ya mfumo wa Umeme kwenye moja kati ya Junction Box lililoko juu ya dari la nyumba hiyo.

UKAGUZI NA UKUSANYAJI WA MADUHULI YA SERIKALI.

Ukaguzi wa kinga na tahadhari ya majanga ya moto umefanyika katika maeneo mbalimbali ya biashara ili kuimarisha usalama wa moto katika maeneo hayo na kukusanya tozo/maduhuli ya serikali.Jumla ya maeneo kumi na sita(16) yenye thamani

ya ***Tsh 2,460,000/=*** yamekaguliwa na kiasi cha ***Tsh 2,640,000/=*** kimekusanywa kutoka katika maeneo ishirini na tatu(23).

ELIMU YA KINGA NA TAHADHARI YA MAJANGA YA MOTO.

Elimu imeendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali ya watu kwenye mikusanyiko na wakati wa ukaguzi ambapo jumla ya watu 112 wamenufaika na Elimu hiyo kwa mchanganuo ufuatao (i) Ukaguzi - 33 (ii) Dawati Kituoni – 02(iii) Matukio ya Moto - 77 inayofanya JUMLA ya Elimu kwa Umma kuwa watu 112.

CHANGAMOTO.

- Kutokuwa na Mtambo wa kuzimia moto, hali inayochelewesha huduma ya uzimaji moto na kufanya maokozi pindi inapotokea.
- Kucheleweshwa kuripotiwa kwa taarifa za matukio ya moto na maokozi pindi yanapotokea.

SHUKURANI

Shukurani kwa Mh.Mkuu wa Wilaya kwa Miongozo, wajumbe wote wa Kamati ya Usalama Wilaya, Taasisi za Umma, binafsi na wadau mbalimbali kwa ushirikiano

wanaoutoa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

Ninaomba kuwasilisha.

A/insp – Mwanshasha M.Mohamedi

K.n.y - Kaimu Mkuu wa Zimamoto na Uokoaji (W) Muheza